JESMA 009

# JARIBIO LA TISA K.C.P.E

## MUHULA WA TATU 2021/2022
## DARASA LA NANE

KISWAHILI
SEHEMU YA KWANZA:
LUGHA

Muda: Saa 1 dakika 40

### SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

### JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**11.** Neno lipi lina silabi saba?

A. Shelabela
B. Aliwasimamishia
C. Walitupelekea
D. Andikia

Jibu sahihi ni C (Walitupelekea)

1 [A] [B] [C] [D]   11 [A] [B] [▬] [D]   21 [A] [B] [C] [D]   31 [A] [B] [C] [D]   41 [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawa na kuwa maswali yote yamo.**

Tovuti: www.jesmapublishersltd.com Barua pepe: jesmapublishers@yahoo.com

009: Jesma Publishers & Education Boosters Ltd. Simu: 0206554346/0202217088/0701545759/0734207811

FUNGUA UKURASA

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299 E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi* **1** *mpaka* **15**. *Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.*

Wananchi ___1___ kupanda miti ___2___ kuna wale wasiolichukulia suala hili kwa uzito ___3___. Hata wale walio na mashamba wanaonekana kukata miti ___4___. Yakini, ___5___; ingawa ukataji huu unaendelezwa kidogo kidogo, athari ___6___ kupuuzwa ___7___. Tutamlaumu nani ___8___ baada ya nchi yetu kugeuka jangwa? Bila shaka tutakuwa ___9___.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | wanakuwa wamehimizwa | walikuwa wamehimizwa | wangekuwa wanahimizwa | wamekuwa wakihimizwa |
| **2.** | japo | lau | almradi | isitoshe |
| **3.** | lifaalo | ifaayo | ufaao | ufaavyo |
| **4.** | kiholela | ndivyo sivyo | kijuujuu | kilalahoi |
| **5.** | Tamaa mbele mauti mauti nyuma | Tone na tone hujaza ziwa | Cheche ndogo hufanya moto mkubwa | Chururu si ndondondo |
| **6.** | lake haliwezi | zake haziwezi | yake hayawezi | yake haziwezi |
| **7.** | vile | kamwe | kweli | sana |
| **8.** | tukiathiriwa | tukiathiri | mkiathirika | mkiathiriwa |
| **9.** | tumetia mrija | tumekufa kikondoo | tumejifunga masombo | tumejipalia makaa |

Shule zilipofungwa, nilikuwa na ___10___ ya kuwaona kaka na dada zangu; yaani ___11___ wangu. Nilifululiza mwendo ___12___ hadi chengoni. Pindi tu ___13___ mnuna wangu alinikimbilia na kunikumbatia. ___14___ wote ___15___ kwa kuniona.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | hari | hima | shime | shauku |
| **11.** | wanuna | maumbu | familia | aila |
| **12.** | moja kwa moja | juu kwa juu | ana kwa ana | bega kwa bega |
| **13.** | nimewasili | niliwasili | nilipowasili | nilivyowasili |
| **14.** | Jamii | Jamaa | Ajinabi | Wakaazi |
| **15.** | ilifurahi | mlifurahi | zilifurahi | walifurahi |

3

**0734579299 E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at
www.schoolsnetkenya.com

*Kuanzia swali la **16** mpaka **30**, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.*

16. Bainisha matumizi ya kiambishi **ji** katika sentensi ifuatayo.
Uporaji wa mali umezidi.
A. Nafsi B. Mtendaji
C. Hali D. Ngeli

17. Upi ni mpangilio sahihi wa maneno katika sentensi ifuatayo:
Ng'ombe wangu ameuzwa lakini wake atauzwa kesho.
A. nomino, kivumishi, kitenzi, kiunganishi, kivumishi, kitenzi, nomino
B. nomino, kiwakilishi, kitenzi, kiunganishi, kivumishi, kitenzi, kielezi.
C. nomino, kivumishi, kitenzi, kiunganishi, kiwakilishi, kitenzi, kielezi.
D. nomino, kivumishi, kitenzi, kiunganishi, kiwakilishi, kitenzi, nomino.

18. Chagua neno lililo tofauti na mengine.
A. Msumeno B. Singe
C. Jiriwa D. Patasi

19. Badili sentensi ifuatayo katika hali ya wingi.
Dalali alilinunua shati katika kiduka hicho.
A. Dalali walinunua mashati katika maduka hayo.
B. Madalali walinunua mashati katika kiduka hicho.
C. Madalali walinunua mashati katika viduka hivyo.
D. Dalali walinunua mashati katika viduka hivyo.

20. Kanusha:
Nyumba iliyobomoka haikujengwa upya.
A. Nyumba ambayo haikubomoka haikujengwa upya.
B. Nyumba iliyobomoka haikujengwa upya.
C. Nyumba isiyobomoka haijajengwa upya.
D. Nyumba iliyobomoka haijajengwa upya.

21. Mkuo ni kwa sabuni na **msoa** ni kwa
A. watalii. B. nzige.
C. milima. D. mtama.

22. Tambulisha sentensi iliyoakifishwa vizuri.
A. Darasa hili, "akasema," Lina wanafunzi watiifu.
B. Darasa hili, "akasema," "lina wanafunzi watiifu.".
C. "Darasa hili," akasema, "lina wanafunzi watiifu."
D. "Darasa hili," akasema, "Lina wanafunzi watiifu."

23. Sentensi hii imetumia tamathali gani za usemi?
Sayo alitii amri ya moyo wake akachana mbuga asidhurike.
A. Sitiari, tashbihi.
B. Tashhisi, nahau.
C. Tashhisi, chuku.
D. Ishara, chuku.

24. Chagua jibu lenye nomino zilizo katika ngeli ya I - ZI pekee.
A. mvua, hofu B. tambi, kuta
C. karatasi, shule D. ndwele, mabele

25. Ni jibu lipi lenye maelezo sahihi?
A. Katikiro ni mhudumu wa ofisi anayepeleka ujumbe.
B. Sogora hutunga na kuimba nyimbo ngomani.
C. Mgema ni mraibu wa pombe ya mnazi.
D. Mjumu ni mtu anayetengeneza vitu kwa chuma.

26. Ukigawa nusu mara tatu utapata.
A. tusui. B. moja unusu.
C. robo. D. sudusi.

27. Bainisha maelezo sahihi.
A. Vua ni kuondoa nguo mwilini lakini fua ni kumsaidia aliye na tatizo.
B. Chunga ni kutenganisha unga na chenga ilhali shunga ni kufukuza kama vile ndege shambani.
C. Zaka ni kutafuta kila mahali lakini saka ni malipo yatolewayo kanisani.
D. Danga ni maziwa ya kwanza ya mnyama lakini tanga ni mkusanyiko wa watu kabla ya mazishi.

28. Zipi ni sauti ghuna pekee?
A. ch, sh, th B. t, d, k
C. l, p, f D. d, ng', z

29. Sentensi '**asingalipewa dawa asingalipona**' ina maana kuwa,
A. akipewa dawa atapona.
B. alipewa dawa bali hakupona.
C. alipona kwa kupewa dawa.
D. hakupewa dawa wala kupona.

30. Ni methali gani inayotumiwa kumhimiza mtu aliye na shida asipoteze matumaini, huenda siku moja akajaliwa kupata neema?
A. Mambo ni kangaja, huenda yakaja.
B. Mchumia juani hulia kivulini.
C. Mguu mtembezi haukosi mwiba.
D. Mkamia maji hayanywi na akiyanywa humsakama.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299 E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at [www.schoolsnetkenya.com](http://www.schoolsnetkenya.com)

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali kuanzia nambari* **31** *mpaka* **40**

Tangu kugunduliwa kwa uele wa UKIMWI, juhudi kubwa zimefanywa ili kutafuta tiba pamoja na kinga zake. Mpaka leo, hamna maendeleo ya kuridhisha japo yapo matumaini makubwa. Zipo hatua nyingi zilizochukuliwa kupambana na uele huu lengo likiwa ni kuudhibiti katika viwango vya chini kabisa. Baadhi ya juhudi ambazo tunaziona ni kupitia kwa matangazo ya kuwatahadharisha vijana dhidi ya mapenzi ya kiholela na nyendo nyingine zinazoweza kuwatumbukiza katika lindi la maambukizi. Dini na madhehebu mbalimbali yanahimiza nyendo zenye maadili kama njia kuu ya kuushinda ukongo huu. Vyombo vya habari aidha vimekuwa katika mstari wa mbele kutangaza kuhusu ugonjwa huu.

Makongomano na warsha mbalimbali nazo zimeandaliwa ambapo mikakati mbalimbali hujadiliwa ili kuona upi unaofaa insani wa jamii mbalimbali. Mikutano ya aina hii nayo hata hivyo inakashifiwa kwa kujikita katika hoteli kubwa za kifahari katika miji mikuu mbali na upeo wa macho wa mwananchi wa kawaida ambaye vikao vyenyewe vinalenga kumwauni. Wale wanadhamiriwa kusaidiwa hawashirikishwi wala kuhusishwa.

Mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali yamejizatiti kupambana na maradhi haya sugu. Pamoja na mashirika haya na makundi ya watu binafsi zipo dawa za kupooza ukongo huu. Waathiriwa nao huzitumia kupunguza athari zake ili kuyarefusha maisha yao. Licha ya kuwepo kwa dawa hizi kuwa wale ambao hawasifaidi kwa vile hawamudu hata gharama ya usafiri ya kujiwasilisha zinakopatikana. Hawa ni wale akina yakhe wanaoishi katika mitaa ya mabanda na wengine wanaoishi vijijini mbali na ustaarabu wa mji. Hata baadhi ya walalahoi hujipata katika hali kama hii. Wachochole wengi **hujiona wenye bahati hata kupata chakula chao mshindio.** Wengi wanaotumia dawa hizi hulalamikia kuona **kisunzi** watumiapo vidonge hivi pasipo kula chochote.

Tunachoona hapa ni kuwa wale wanaojishughulisha na vita dhidi ya ugonjwa huu hatari wanalenga tu namna ya kuuzuia. Hawatilii maanani njia za kuwahudumia wahasiriwa wenyewe. Hawa wanaelekea kutelekezwa kabisa na mashirika husika pamoja na jamaa zao ambao huwaona kama mzigo mkubwa kwao. Umefika sasa wakati wa kushughulikia ndugu zetu hawa kwa mapenzi ya dhati.

Serikali za nchi za kiafrika zinafaa kutoa dawa kwa bei nafuu ili kuwawezesha wananaougua kukabiliana na maradhi ainati ambayo huwanyemelea kinga yao inapodhoofika. Waja hawa wanaweza kupata bahati ya kuyasukuma mbele maisha ya vitoto vyao vikembe hadi vikaweza kujiangalia vyenyewe. Waathirika hawatakuwa wamenufaika kwa msaada huu peke yao tu bali pia watoto wanaowategemea. **Mzazi anapotuacha mkono mwanawe huathirika sana.** Wagonjwa hawa wasipuuzwe kama kwamba wanashutumiwa kwa kuugua uele huu.

Ni wajibu wa kila mmoja wetu kujikinga na ugonjwa huu na vilevile kuwanyoshea mkono wa msaada wanaougua



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299 E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at [www.schoolsnetkenya.com](http://www.schoolsnetkenya.com)

31. Chagua kauli iliyo sahihi.
A. Juhudi za kuvumbua kinga ya UKIMWI zimeambulia patupu.
B. Tiba dhidi ya UKIMWI imeweza kuvumbuliwa sasa.
C. Mafanikio makubwa yamepatikana dhidi ya maradhi ya UKIMWI .
D. Wadau wana matumaini ya kupata tiba ya Ukimwi.

32. Walio katika hatari kubwa zaidi ya kuambukizwa uele huwa hasa ni,
A. watoto wasiojua kujilinda.
B. watu wazima.
C. vijulanga wasiowajibika.
D. wazee na watu wa makamu.

33. Njia bora zaidi ya kuudhibiti uele huu na maambukizi yake kwa mujibu wa viongozi wa kidini ni,
A. kujistahi na kuwa na hulka bulibuli.
B. kuzingatia maadili na hulka benibeni.
C. kutumia kinga na kufanya ibada.
D. kukiuka maadili na tabia ya uasherati.

34. Makongamano mengi hayajaweza kuzaa matunda yafaayo. Hili linatokana na yote haya **ila**,
A. kuandaliwa mbali na wanaonuiwa kufaidika.
B. kufanyika katika maeneo yalio marufuku kwa wachochole.
C. kutoshikirikisha makundi yanayonuiwa kufaidika.
D. kutowekewa mikakati ifaayo ili wote wahusishwe.

35. Dawa zilizopo kwa sasa ni muhimu kwa,
A. kuzuia virusi vya UKIMWI visiingie mwilini.
B. kuua virusi vya UKIMWI kwa kiasi fulani.
C. kupunguza kasi ya kuenea kwa virusi mwilini.
D. kuongeza chembechembe za kuua virusi hivi.

36. **Huwa ni bahati hata kupata chakula cha mshindio** maana yake ni kuwa,
A. wananchi wanaougua hushindwa kula zaidi ya mara moja kwa siku.
B. wale wanaougua huona ugumu kula mara moja tu kwa siku.
C. baadhi ya wahasiriwa hutaabika kiasi cha kukosa kula hata mara moja kwa siku.
D. wahasiriwa wengine huwa wahitaji kiasi cha kushindwa kupata hata mlo mmoja kwa siku.

37. Katika aya ya nne, mwandishi anapendekeza
A. juhudi zielekezwe kwa wanaougua kama zile za kuzuia.
B. mafunzo zaidi yatolewe ili kupunguza maenezi ya UKIMWI.
C. Tujizatiti zaidi kuwasaidia wanaougua kuliko kukabiliana na maambukizi.
D. Wanaougua watelekezwe ili kupunguza athari zaidi za uele huu.

38. **Mzazi anapotuacha mkono mwanawe huathirika sana**?
Ni methali ipi inayotilia mkazo kauli hii?
A. Upweke ni uvundo.
B. Mti mkuu ukigwa wana wa ndege huyumba.
C. Mama ni mama ajapokuwa rukwama.
D. Uchungu wa mwana aujuaye mzazi.

39. Juhudi za kukabiliana na maradhi ya UKIMWI zitafanikishwa zaidi na,
A. vijana katika jamii.
B. serikali za Kiafrika.
C. wanajamii wote.
D. wale walioathirika.

40. Kuona **kisunzi** ni sawa na kuona;
A. riahi
B. kigugumizi
C. fedheha
D. kisulisuli

*Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali kuanzia* **41** *mpaka* **50**

Mishale ya saa ilikuwa karibu kuashiria saa saba kamili. Mapuya alinyanyuka za kuranda hapa na pale katika chumba chake kilichokandikwa kwa udongo na samadi. Chakula cha mchana kilikuwa kimechelewa na alikuwa na shaka iwapo kweli atawahi au wenzake watakuwa wamemmalizia. Alimwita mkewe ambaye alimwambia asubiri kidogo kwani alikuwa katika hatua za mwisho za kukiandaa chakula. "Hii ndiyo tabia yako," Mapuya alimfokea mkewe, "Wanaume wengine waliisha kupikiwa mapema na wewe mpaka sasa huna unalofanya." Maneno hayo yalimkata ini mkewe ambaye mgongo ulimwuma kwa kuupinda kwa shughuli za hapa na pale tangu asubuhi aliporauka.

Licha ya kuumizwa na maneno yale, mkewe hakutaka kukorofishana na mume wake. Alionelea vyema afuate mkondo mwingine. Alimwambia mumewe kwa upendo, "Mume wangu, mimi najitahidi sana hapa. Naona tatizo ni wewe kuwa mtumwa wa ugimbi. Siwezi kukuzuia kwa lazima usinywe pombe hiyo ila mimi kila utokapo hapa nyumbani huwa nina wahaka iwapo utarejea mzima."

"Wasiwasi? Hivi mimi ni mtoto? Naona umeanza kumea pembe wewe." "Hata! mie nakupa masaha tu. Pombe hii ya bei nafuu imewafanya wanaume wengi kuwa mazuzu tu! **Hawajijui hawajitambui**. Umewaona vijana wengi huku kwetu wanaokwenda wakipepesuka utadhani ni mmea ulionyauka baada ya mzizi wake mkuu kuliwa na fuko wakati wa kiangazi. Babu zao wana siha kuwashinda, shughuli nyingi tayari zimekwama kwa kukosa watendaji."

Baada ya haya kusemwa, Mapuya alikurupuka na kuenda zake. Hakutaka kukisubiri chakula ambacho sasa kilikuwa tayari wala kumsikiliza mkewe. Njia aliyoshika ilimwongoza hadi katika kibanda kimoja ambapo sauti nzito za wanaume zilisikika zikivuma ungedhani ni sauti za nyuki mzingani.

Waja waliingia na kujazana kote. Vicheko vilipamba moto huku watu wakinong'onezana katika vikundi. Nyimbo nazo zilinoga. Ni katika kilele hiki ambapo mmoja alilalamikia kuumwa kichwa. Wenzake waliyaona haya kama masihara. Alipoanza kulia, walianguka kicheko na kudhani kuwa ulevi ndio uliokuwa ukimliza. Muda mfupi baadaye, bwana mmoja alisikika akisema, 'Giza limeingia ghafla, washeni taa." Watu walizidi kucheka kwa kuona sinema, Idadi ya waliotaka taa kuwashwa ilizidi kuongezeka.

Baadhi ya watu, akiwemo Mapuya, walianza kukumbuka visa kadhaa vya upofu vilivyowakumba watu waliobugia ugimbi wa sampli hii. Kila mmoja aliondoka taratibu akiwa amejikunja kuelekea kwake. Kilichomsumbua Mapuya ni maneno aliyokuwa amemwambia mkewe kabla ya kuondoka ghafla kiamboni mwake. Yalimvamia na kumtesa. Alitaka sana kuwasili manzilini kuiona jamaa yake. Njia ndiyo iliyomtesa zaidi kwani aliiona kuwa ndefu mara kumi kuliko urefu wake wa kawaida. Alichelea kufikwa na wenzake kabla ya kuwahi kwake.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299 E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

41. Tukio hili lilitokea majira yapi?
A. Adhuhuri
B. Macheo
C. Machwa
D. Magharibi

42. Taharuki aliyokuwa nayo Mapuya ilitokana na;
A. kuchelewa kwa chakula chake cha mchana.
B. hamu ya kufika ulevini pasipo kukawia.
C. tabia ya mkewe ya kuchelewesha chakula.
D. hofu ya kufika mkutanoni baada ya wenzake.

43. Bi Mapuya alipomtajia mumewe kuhusu ulevi wake;
A. alitaka kulipiza kisasi kwa maneno ya mumewe.
B. alikuwa kama wake wengine waliowabughudhi waume wao.
C. alitaka kumwudhi ili aghairi kuenda ulevini.
D. alihitaji kudhihirisha tu kwamba alimjali sana mumewe.

44. "**Hawajijui hawajitambui**" hii ni fani gani ya lugha?
A. Vielezi vya mkazo.
B. Tanakali za sauti.
C. Kinaya
D. Methali

45. Madhara mawili ya pombe yanayojitokeza katika kifungu hiki ni
A. kuathiri siha, kuvunjika kwa familia.
B. kukosa hamu ya kula, kupenda kugombana.
C. kusababisha ulemavu, kudhoofisha utendakazi.
D. kupumbaza akili, kuzeeka kuliko mababu.

46. Jambo lipi **SI** kweli kulingana na aya ya saba?
A. Baadhi ya watu waliongea kwa sauti za chini.
B. Walevi wote waliongea kwa sauti za juu sana.
C. Kupuuza madhara yanapoanza kujitokeza kunaweza kusababisha kuathirika kwa wengi zaidi.
D. Ulevi ulipokithiri wengi walianza kulia wakiomba kuwashiwa taa.

47. Inaonekana wazi kuwa,
A. Mapuya na wenzake hawakuyajua madhara ya pombe.
B. Ulevi uliwafanya Mapuya na wenzake kukumbuka visa vya upofu.
C. huenda matukio ya aina hii yaliwahi kutokea hapo awali.
D. watu waliojionea sinema ya bure walicheka taa zilipowashwa.

48. Yule aliyeomba kuwashiwa taa kwanza
A. alikuwa amelewa kiasi cha kutoona vizuri.
B. alikuwa na maumivu makali kichwani.
C. alichekwa kwa kuwa wenzake walivizoea vitimbi vyake.
D. alizichukulia dalili za upofu kuwa ni giza lililoingia.

49. Upi ni mfuatano wa matukio katika kifungu hiki?
A. Chakula kuchelewa, kushauriwa, kilio, vicheko, kufumukana.
B. Kugombana, chakula kuchelewa, ulevi, vicheko, kufika nyumbani.
C. Kugombana, kuondoka ghafla, vicheko, kilio, kuelekea kibandani.
D. Kujiunga ulevini, nyimbo, vicheko, kilio, visa vya upofu.

50. Kifungu kimesema yote haya **ila**?
A. Mapuya aliyajutia maneno aliyomwambia mkewe.
B. Mapuya aligundua kuwa jamaa ni muhimu kwake.
C. Njia ilikuwa refu kuliko kawaida siku hiyo.
D. Mapuya alihofia kufikiwa na madhara akiwa njiani.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299 E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com